# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA TATU

**10 APRILI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA TATU – TAREHE 10 APRILI, 2025

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**31. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini ahadi ya Serikali ya kujenga Wodi Kituo cha Afya Kihagara itatekelezwa ili kuondoa changamoto kubwa iliyopo.

**32. MHESHIMIWA AMANDUS JULIUS CHINGUILE (NACHINGWEA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo Nachingwea kuwa Mamlaka ya Mji.

**33. MHESHIMIWA DKT. MEDARD MATOGOLO KALEMANI (CHATO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakarabati Shule kongwe za Msingi katika Jimbo la Chato.

**34. MHESHIMIWA FELISTA DEOGRATIUS NJAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Msinga hadi Masoka ili kupunguza adha kwa Wananchi wa Moshi Vijijini.

**WIZARA YA NISHATI:**

**35. MHESHIMIWA REUBEN NHAMANILO KWAGILWA (HANDENI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina maelezo gani juu ya kero sugu ya kukatika umeme mara kwa mara Handeni Mjini na lini kero hiyo itatatuliwa.

## WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

**36. MHESHIMIWA JUSTIN LAZARO NYAMOGA (KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itajenga minara ya mawasiliano Vijiji vya Lukani na Ng'uluhe - Kilolo ili kuboresha mawasiliano.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

**37. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa kisasa utaanza Mkoani Njombe.

**WIZARA YA UJENZI:**

**38. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ipo tayari kutenga fedha za ujenzi wa kilomita chache Barabara ya Lupiro, Malinyi, Kilosa kwa Mpepo na Namtumbo ambayo ni Ilani ya CCM.

**39. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Njombe, Kibena, Madeke, Lupembe kuelekea Mkoa wa Morogoro.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**40. MHESHIMIWA KAVEJURU ELIADORY FELIX (BUHIGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Viwanda vya kuchakata zao la Migomba.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA**
**10 APRILI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**